**KISWAHILKI KARATASI YA KWANZA**

## SEHEMU YA A

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 1–7**

Familia ya Bi. Njeri ilikuwa imepanga kuitembelea Hifadhi ya Taifa ya Tsavo kwa muda mrefu. Hatimaye, wakati wa likizo ya Disemba, ndoto hiyo ilitimia. Waliondoka nyumbani asubuhi na mapema wakiwa wamejaa shauku ya kukutana ana kwa ana na wanyama pori.

Watoto wake wawili, Wanjiru na Kimani, walikuwa wakisoma katika darasa la saba na la nane mtawalia. Walikuwa wamesoma kuhusu simba, tembo na twiga vitabuni lakini hawakuwahi kuwaona moja kwa moja.

Siku ya pili walipotembelea hifadhi hiyo, waliona kundi kubwa la tembo wakinywa maji mtoni. Tembo mmoja alikuwa na ndama wake na aliwahimiza wanawe kuwa watulivu. Kwa mbali, walimwona simba akiwa amejificha kwenye nyasi akimvizia swara aliyekuwa akila majani kwa utulivu.

Watoto walishangaa kuona jinsi wanyama hao walivyokuwa wakitegemeana kwa uhai.

Zaidi ya hayo, walitembelea kambi ya wageni ambapo walijifunza kuhusu juhudi zinazofanywa na wahifadhi kuwalinda wanyama dhidi ya uwindaji haramu na ukataji miti kiholela.

Wakati wa kuondoka, familia hiyo ilishiriki kupanda miti kama mchango wao wa kuhifadhi mazingira. Safari hiyo ilibadili mtazamo wao kuhusu umuhimu wa asili na uhifadhi.

1. Kwa nini familia ya Bi. Njeri iliamua kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Tsavo?

A. Walitaka kujiunga na wahifadhi wa mazingira
B. Ilikuwa ndoto yao ya muda mrefu
C. Walikuwa wakitoroka jiji
D. Walikuwa wamealikwa rasmi

2. Wanjiru na Kimani walikuwa katika madarasa gani?

A. Tano na sita  B. Sita na saba
C. Saba na nane  D. Tisa na kumi

3. Kwa nini watoto walishangaa walipomwona simba?

A. Walikuwa na hofu ya kushambuliwa
B. Walikuwa wamezoea kuona simba kwenye runinga tu
C. Simba alikuwa amevaa mbugani
D. Simba alikuwa akimvizia swara

4. Tembo waliokuwa wakinywa maji walionyesha nini kuhusu maisha ya wanyama?

A. Woga wa binadamu
B. Uadui wa asili
C. Upendo na malezi
D. Mapambano ya kila mara

5. Watoto walijifunza nini katika kambi ya wageni?

A. Jinsi ya kuendesha magari ya mbuga
B. Umuhimu wa uwindaji wa kiasili
C. Hatari ya uwindaji haramu na ukataji miti
D. Utalii wa kimataifa

6. Familia hiyo ilionyesha mchango wao kwa mazingira kwa:

A. Kufanya usafi wa hifadhi
B. Kupanda miti
C. Kuchora picha za wanyama
D. Kurekodi video za mbuga

7. Mtazamo wao kuhusu mazingira ulibadilika vipi baada ya safari?

A. Waliona mazingira si muhimu
B. Walifurahia kula nyama pori
C. Walitambua umuhimu wa kuhifadhi mazingira
D. Walivutiwa kuanzisha biashara ya utalii



**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 8–14**

Kijiji cha Mwangaza kilijulikana kwa mashamba makubwa ya mahindi na maharagwe, lakini kilikumbwa na tatizo sugu la ukosefu wa maji safi. Kwa miaka mingi, wakaazi walilazimika kutembea zaidi ya kilomita tano kila siku kwenda mtoni kuteka maji.

Mto huo ulikuwa umejaa uchafu hasa wakati wa mvua ambapo tope na takataka kutoka maeneo ya juu yalipelekwa humo.

Hali hii iliwaathiri zaidi watoto waliokuwa wakihitajika kusaidia kuteka maji kabla ya kwenda shule. Mara kwa mara walichelewa au kukosa masomo kabisa.

Kwa usaidizi wa serikali ya kaunti na shirika moja lisilo la kiserikali, mradi wa kuchimba visima ulianzishwa. Baada ya miezi mitatu ya uchimbaji na mafunzo kuhusu matumizi salama ya maji, visima viwili vilianza kutoa maji safi.

Furaha ilienea kijijini; watoto walirudi shuleni, shughuli za kilimo zilipata msukumo mpya na maisha kwa ujumla yalibadilika.

8. Tatizo kuu lililokuwa likiwakumba wakazi wa Kijiji cha Mwangaza ni:

A. Ukosefu wa maji safi
B. Kutengwa kwa jamii
C. Ukosefu wa chakula
D. Uhalifu mwingi

9. Athari mojawapo ya tatizo hilo kwa watoto ni:

A. Walianzisha biashara ya maji
B. Walihamia miji ya mbali
C. Walikosa kuhudhuria masomo ipasavyo
D. Walipata kazi ya uchimbaji wa visima

10. Mto uliokuwa karibu na kijiji ulipataje uchafu?

A. Kutoka viwandani
B. Kutokana na magonjwa ya wanyama
C. Kutokana na mvua iliyoleta tope na takataka
D. Kutoka kwa watu waliokuwa wakioga

11. Serikali ya kaunti ilifanya nini kusaidia?

A. Ilituma walimu wa afya
B. Ilipeleka chakula cha msaada
C. Iliunda tume ya uokoaji
D. Ilishirikiana kuchimba visima

12. Baada ya visima kukamilika, maisha ya wanakijiji yalibadilika vipi?

A. Watoto walirudi shuleni na kilimo kikaimarika
B. Walienda mijini kufanya kazi
C. Watoto walihamia shule za bweni
D. Walianzisha kilimo cha maua

13. Mradi wa kuchimba visima ulidumu kwa muda gani?

A. Wiki mbili
B. Mwezi mmoja
C. Miezi miwili
D. Miezi mitatu

14. Lengo la mafunzo kwa wanakijiji lilikuwa:

A. Jinsi ya kuuza maji
B. Matumizi salama ya maji
C. Uundaji wa mabomba ya maji
D. Njia za kuongeza mapato

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 15–20**

Katika kijiji cha Mji Mpya kulikuwa na kijana mmoja aliyejulikana kwa jina la Bakari. Alikuwa fundi mchanga lakini hodari sana katika kutengeneza samani za mbao.



Mwanzoni watu walimdharau kwa sababu alikuwa mchanga na hakuwa na duka kubwa la kisasa. Hata hivyo, kwa ustadi wake kazi zake zilianza kuvutia watu wengi.

Alizingatia maadili ya kazi kama vile uaminifu, ubora na kuheshimu muda wa mteja. Hata shule ya msingi ya kijiji ilimwajiri kutengeneza madawati mapya.

Bakari hakuwahi kuwa na kiburi bali alitumia mafanikio yake kuwashauri vijana kuhusu umuhimu wa bidii na kujituma.

15. Bakari alikuwa na ujuzi wa kazi gani?

A. Uchuuzi wa bidhaa
B. Uchoraji wa picha
C. Utengenezaji wa samani
D. Upishi wa chakula

16. Kwa nini watu walimdharau mwanzoni?

A. Alikuwa na deni kubwa
B. Alikuwa mchanga na hakuwa na duka kubwa
C. Alitoka mji mwingine
D. Hakuwahi kwenda shule

17. Wateja wake walibadilika vipi baada ya kuona kazi yake?

A. Walimwajiri mashambani
B. Waligeuka kuwa wateja wa kudumu
C. Walimkashifu zaidi
D. Walimlalamikia bei

18. Shule ya msingi ilimwajiri Bakari kufanya nini?

A. Kufundisha sanaa
B. Kupamba ofisi ya mwalimu mkuu
C. Kutengeneza madawati mapya
D. Kuwashauri wanafunzi

19. Bakari alijenga nini kusaidia vijana?

A. Shule ya upili
B. Karakana ndogo ya mafunzo
C. Soko la samani
D. Ghala la vifaa

20. Kulingana na Bakari, mafanikio yanategemea nini?

A. Ubahili na ujanja
B. Urafiki na serikali
C. Nidhamu, subira na lengo
D. Elimu ya chuo kikuu pekee

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali 21–25**

**Juma:** Hujambo, Halima? Nimesikia kesho kuna mkutano wa wazazi shuleni. Umeshapokea mwaliko?

**Halima:** Sijambo, Juma. Ndiyo, nilipokea ujumbe jana kutoka kwa mwalimu mkuu kupitia kwa mtoto wangu.

**Juma:** Nilikuwa nasikia minong'ono kuhusu nidhamu ya wanafunzi na kushuka kwa viwango vya ufaulu.



**Halima:** Ni kweli. Walimu wamekuwa wakilalamikia kuchelewa kwa wanafunzi, utoro na baadhi yao kuja shuleni bila sare.

**Juma:** Inabidi tushirikiane na walimu ili kusaidia watoto wetu.

**Halima:** Pia kutakuwa na kikao kuhusu ada za shule na kuboresha maktaba.

21. Mazungumzo haya yanafanyika kati ya nani?

A. Walimu wawili
B. Juma na Halima
C. Watoto wawili
D. Mwalimu na mwanafunzi

22. Ni sababu ipi iliyotajwa kama chanzo cha mkutano?

A. Sherehe ya mwisho wa mwaka
B. Changamoto za nidhamu na ufaulu
C. Kuandaa orodha ya wanafunzi wapya
D. Ujenzi wa bweni

23. Mkutano utafanyika wapi na saa ngapi?

A. Ofisini saa mbili
B. Ukumbi wa shule saa tatu asubuhi
C. Maktaba saa tano asubuhi
D. Uwanjani saa sita mchana

24. Mbali na masuala ya nidhamu, mkutano utajadili nini?

A. Michezo ya shule
B. Safari za wanafunzi
C. Ada za shule na maktaba
D. Chakula cha wanafunzi

25. Halima anashauri nini?

A. Mkutano uahirishwe
B. Ujadiliwe mitandaoni
C. Wazazi wafanye maandamano
D. Wazazi wafike kwa wakati na washirikiane na walimu

**Jaza nafasi kwa kuchagua jibu sahihi Maswali 26–35**

Mawasiliano ni sekta mojawapo **(26)** _________ hatua sana **(27)** _________ kuvumbuliwa kwa teknolojia mpya. Siku hizi hata **(28)** _________ waliotumika sana kupokea na kupeleka ujumbe na barua wamejipata hawana lao.

Ulimwengu umekuwa kama duara **(29)** _________ habari huweza kusambaa **(31)** _________ katika muda mfupi sana. Hata hivyo, hapana marefu yasiyokuwa na **(32)** _________. Watu wenye nia mbaya wanatumia nafasi hiyo kueneza uvumi **(33)** _________ wengine wakisambaza picha zisizofaa mitandaoni.

Iwapo teknolojia hii itatumiwa vizuri, basi itakuwa **(34)** _________ kubwa kwa maendeleo ya jamii. Kwa hivyo, ni muhimu kila mmoja wetu kuwa na **(35)** _________ ya kutumia vyema mitandao ya kisasa.



| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 26 | zilizopiga | yaliyopiga | tulizopiga | iliyopiga |
| 27 | hadi | kama | tangu | kuliko |
| 28 | matarishi | masogora | mabawabu | masakubimbi |
| 29 | dogo | ndogo | kidogo | mdogo |
| 30 | bali | kwani | lau | huku |
| 31 | zote | yote | mwote | kote |
| 32 | ncha | baraka | ndume | mwenzake |
| 33 | huku | ilhali | bali | lakini |
| 34 | hasara | suluhisho | baraka | adhabu |
| 35 | malengo | maamuzi | mipango | nidhamu |

***Kuanzia swali la 36 hadi la 50, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.***

36. Ufanisi hauwezi kupatikana _______ umoja.

A. lau
B. minghairi ya
C. isipokuwa
D. madhali

37. Mafiga _______ ndiyo yaliyotumiwa jana.

A. yaya haya
B. haya yaya
C. haya haya
D. yaya yaya

38. Bainisha kielezi katika sentensi:

*Walionywa dhidi ya kuuza ardhi yao kiholela.*

A. dhidi ya B. yao
C. kiholela D. ardhi

39. Kanusha:

*Matayo alivunjika mguu akatibiwa.*

A. Matayo aliyevunjika mguu hakutibiwa.
B. Matayo hakuvunjika mguu wala kutibiwa.
C. Matayo hakuvunjika mguu akatibiwa.
D. Matayo hajavunjika mguu wala hatatibiwa.

40. Chagua sentensi sahihi.

A. Angalijua pana wezi angefunga mlango.
B. Angejua pana wezi angalifunga mlango.

C. Angelijua pana wezi angefunga mlango.
D. Angalijua pana wezi angalifunga mlango.

41. *Paulo ni sungura.*

Sentensi hii imetumia:

A. Sitiari
B. Tashbihi
C. Nahau
D. Tanakali za sauti

42. Geuza katika kauli ya kutendwa:

*Lucy alikivunja kioo cha Daudi.*

A. Daudi alivunjiwa kioo na Lucy.
B. Kioo kilivunjiwa Daudi na Lucy.
C. Kioo cha Daudi kilivunjwa na Lucy.
D. Lucy alimvunjia Daudi kioo chake.

43. Andika kwa wingi:

*Ufa wa ukuta huu ni mpana.*

A. Nyufa ya kuta hii ni mipana.
B. Nyufa za kuta hizi ni pana.
C. Nyufa za kuta hii ni pana.
D. Nyufa za nyuta hizi ni pana.

44. Badili katika usemi wa taarifa:

*"Wageni wetu watawasili kesho," baba alisema.*

A. Baba amesema kuwa wageni wetu wangewasili kesho.
B. Baba angesema kuwa wageni wetu watawasili kesho.
C. Baba anasema kuwa wageni wetu watawasili siku ifuatayo.
D. Baba alisema kuwa wageni wetu wangewasili siku ambayo ingefuata.

45. Msemo **"kupiga milundi"** una maana ya:

A. Kukimbia
B. Kuogelea
C. Kuimba
D. Kutembea

46. Ni jozi ipi yenye nomino za ngeli ya LI-YA pekee?

A. Jua, ndizi
B. Ua, jembe
C. Meza, karatasi
D. Vumbi, shule



47. Tegua kitendawili:

*Watu huitembelea nyumba yangu lakini hawapendi kuingia.*

A. Yai
B. Bahari
C. Msalani
D. Kaburi

48. Bainisha sentensi iliyoakifishwa ipasavyo.

A. Rununu, simu ya mkononi, imerahisisha mawasiliano.
B. Alinunua nyanya, mboga, vitunguu, na viazi.
C. Lo, umetoka mjini kwa miguu?
D. Wametueleza ukweli........hatuna haja ya ugomvi.

49. Neno **"walinunua"** ni:

A. Kitenzi cha wakati uliopo
B. Kivumishi
C. Kitenzi cha wakati uliopita
D. Nomino ya kawaida

50. Nomino ya pekee ni ipi?

A. Mtoto
B. Shungi
C. Nairobi
D. Upendo

KISWAHILI KARATASI YA KWANZA – MAJIBU

SEHEMU YA A:

Kifungu 1 (1–7)

1. **B. Ilikuwa ndoto yao ya muda mrefu**
2. **C. Saba na nane**
3. **B. Walikuwa wamezoea kuona simba kwenye runinga tu**
4. **C. Upendo na malezi**
5. **C. Hatari ya uwindaji haramu na ukataji miti**
6. **B. Kupanda miti**
7. **C. Walitambua umuhimu wa kuhifadhi mazingira**



Kifungu 2 (8–14)

8. **A. Ukosefu wa maji safi**
9. **C. Walikosa kuhudhuria masomo ipasavyo**
10. **C. Kutokana na mvua iliyoleta tope na takataka**
11. **D. Ilishirikiana kuchimba visima**
12. **A. Watoto walirudi shuleni na kilimo kikaimarika**
13. **D. Miezi mitatu**
14. **B. Matumizi salama ya maji**

Kifungu 3 (15–20)

15. **C. Utengenezaji wa samani**
16. **B. Alikuwa mchanga na hakuwa na duka kubwa**
17. **B. Waligeuka kuwa wateja wa kudumu**
18. **C. Kutengeneza madawati mapya**
19. **B. Karakana ndogo ya mafunzo**
20. **C. Nidhamu, subira na lengo**

Mazungumzo (21–25)

21. **B. Juma na Halima**
22. **B. Changamoto za nidhamu na ufaulu**
23. **B Ukumbi wa shule saa tatu asubuhi**
24. **C. Ada za shule na maktaba**
25. **D. Wazazi wafike kwa wakati na washirikiane na walimu**

SEHEMU YA B:

26. **A. zilizopiga**
27. **C. tangu**
28. **A. matarishi**
29. **B. ndogo**
30. **B. kwani**
31. **D. kote**

32.**A. ncha**
33.**D. lakini**
34.**C. baraka**
35.**D. nidhamu**

MASWALI 36-50

36.**C. isipokuwa**
37.**C. haya haya**
38.**C. kiholela**
39.**B. Matayo hakuvunjika mguu wala kutibiwa**
40.**B. Angejua pana wezi angalifunga mlango**
41.**A. Sitiari**
42.**C. Kioo cha Daudi kilivunjwa na Lucy**
43.**B. Nyufa za kuta hizi ni pana**
44.**D. Baba alisema kuwa wageni wetu wangewasili siku ambayo ingefuata**
45.**A. Kukimbia**
46.**B. Ua, jembe**
47.**D. Kaburi**
48.**C. Lo, umetoka mjini kwa miguu?**
49.**C. Kitenzi cha wakati uliopita**
50.**C. Nairobi**